

336/2 LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI

KIDATO CHA TATU (S.3)

SEHEMU A

UFAHAMU

1. Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

NJIA YA KUTOKEA

Katika kijiji cha Mwangaza, aliishi kijana mmoja aitwaye Juma. Juma alikuwa mwerevu darasani lakini alijikuta akishawishiwa na marafiki waliomvuta katika janga la madawa ya kulevya. Alianza kwa kuvuta bangi na tubaku akiamini kuwa ilikuwa njia ya kupata furaha na kujisikia huru. Kadiri muda ulivyosonga, alizoea heroini na kokeini, hali iliyomfanya kuwa tegemezi wa madawa hayo.

Juma alianza kuiba nyumbani ili apate pesa za kununua madawa ya kulevya kama miraa, na mafura ya magari. Wazazi wake walijaribu kumshauri, lakini hakuwa tayari kusikia. Aliacha shule na kujiingiza katika uhalifu ili kupata fedha. Maisha yake yalibadilika; akawa dhaifu na mwili wake ulianza kudhoofika. Watu wa kijijini walimkwepa kwa sababu ya tabia yake mbaya.

Siku moja, alikutana na mzee mmoja aitwaye Bwana Kombo, ambaye alikuwa mshauri wa vijana. Bwana Kombo alimweleza kuhusu madhara ya madawa ya kulevya na jinsi ambavyo angeweza kuacha. Alimpeleka kwenye kituo cha marekebicho ya tabia ambapo alipata matibabu na ushauri. Baada ya miezi kadhaa, Juma alirudi nyumbani akiwa mtu mpya. Alianza kampeni ya kuhamasisha vijana kuhusu madhara ya madawa ya kulevya. Kwa msaada wa jamii, alirejea shuleni na hatimaye kuwa mshauri wa vijana wengine.

MASWALI

1. Taja sababu mbili zilizomfanya Juma kujiingiza katika matumizi ya madawa ya kulevya.
2. Eleza matokeo / athari mabaya yaliyompata Juma baada ya kuanza kutumia madawa ya kulevya.
3. Mzee Kombo alimsaidia vipi Juma
4. Kwa maoni yako, ni njia gani nyingine zinazoweza kutumika kuwasaidia/ kuzuia vijana wanaotumia madawa ya kulevya?
5. Taja mifano ya madawa ya kulevya ambayo hutumiwa na juma kulingana na hadithi.

Soma shairi halafu jibu maswa utakayopewa

AFRIKA MAMA YETU

Amkeni kila pembe, sasa kumepambazuka
Twanyanyaswa kama ng'ombe, hali giza latoweka
Damu moto tujisombe, sote wana Afrika
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika
Afrika ni mama yetu, hata ikiwa na maradhi

Kwenye heri au shari, ukombozi tunataka
Bara lote liwe huri, Afrika kutukuka

Ubaguzi ni hatari, ni unyama wa tabaka
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika
Afrika ni mama yetu ,hata ikiwa na maradhi

Tukomboe bara letu, viongozi wasifika
Dumisha umoja wetu, nchi huru Afriak
Umoja ni ngao yetu, hatutaki kutengeka
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika
Afrika ni mama yetu, hata ikiwa na maradhi

Sote tunajua vyema, mama yetu Afrika
Tena tumpe uzima, kubwa usiopimika
Kwa kuondoa unyama, wa kusi na vibaraka
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika
Afrika ni mama yetu hata ikiwa na maradhi

Vijana tangulieni, mbele bila kugeuka
Misiri hadi Kusini, Mulikeni Afrika
Kaburu na mahaini, kuwatia hekaheka
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika
Afrika ni mama yetu , hata ikiwa na maradhi

Ukoloni- mamboleo, na ubwana tumechoka
Wenyeji na wengineo, ni mabomu kufyatuka
Maovu si marejeo, tusirudi tukotoka
Afrika ni mama yetu , hata ikiwa na maradhi

MASWALI.

1. Chambua muundo wa shairi hili.
- 2 Taja maudhui yanayopatikana katika shairi

- MWISHO -

Nawapendeza likizo mwanana.